



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TUME YA VYUO VIKUU TANZANIA



TAARIFA KWA UMMA

KUKAMILIKA KWA AWAMU YA KWANZA NA KUFUNGULIWA KWA AWAMU YA PILI YA UDAHILI WA SHAHADA YA KWANZA KWA MWAKA WA MASOMO 2020/2021

Dar es Salaam, 9 Oktoba, 2020

1.0 KUKAMILIKA KWA AWAMU YA KWANZA YA UDAHILI 2020/2021

Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU) inapenda kufahamisha umma na wadau wote wa Elimu ya Juu nchini kuwa awamu ya kwanza ya udahili kwa ngazi ya Shahada ya Kwanza katika Taasisi za Elimu ya Juu kwa mwaka wa masomo 2020/2021 imekamilika. Majina ya waliodahiliwa katika awamu hii yanatangazwa na vyuo husika.

Katika Awamu hii ya Kwanza ya udahili kwa mwaka wa masomo 2020/2021, jumla ya waombaji **90,572** wametuma maombi ya kujiunga katika vyuo **74** vilivyoidhinishwa kudahili. Aidha, jumla ya programu **686** zimeruhusiwa kudahili ikilinganishwa na programu **645** mwaka 2019/2020. Vilevile kwa upande wa nafasi, mwaka huu kuna jumla ya nafasi **157,770** ikilinganishwa na nafasi **149,809** mwaka uliopita. Hili ni ongezeko la nafasi **7,961** za Shahada ya Kwanza sawa na asilimia **5.3**.

Pia katika Awamu hii ya Kwanza ya udahili, jumla ya waombaji **60,621** sawa na asilimia **69.9** ya waombaji walioomba udahili wameshapata udahili vyuoni. Mwenendo wa udahili wa Awamu ya Kwanza kwa kipindi cha miaka mitatu (2018/2019 hadi 2020/2021) unaonesha ongezeko kubwa la waombaji ikiashiria ongezeko la wahitimu wa Kidato cha Sita na wale wa Stashahada. Mchanganuo wa mwenendo wa udahili kwa Awamu za Kwanza kwa kipindi cha miaka mitatu umeainishwa katika **Jedwali Na.1**.

Jedwali Na. 1 Mwenendo wa Udahili kwa Awamu ya Kwanza kwa Kipindi cha Miaka Mitatu 2018/19 – 2020/21

Na.	Maelezo	Idadi kwa Mwaka wa Masomo		
		2018/19	2019/20	2020/21
1.	Jumla ya Waombaji	74,113	83,197	90,572
2.	Waliodahiliwa	43,005	51,385	60,621
3.	Wasiudahiliwa	31,108	31,812	29,951
4.	Waliodahiliwa Chuo kimoja	26,898	30,527	32,120
5.	Waliodahiliwa zaidi ya Chuo kimoja	16,507	20,858	28,501

2.0 WAOMBAJI WALIODAHILIWA KATIKA CHUO ZAIDI YA KIMOJA

Waombaji waliodahiliwa katika chuo zaidi ya kimoja wanahimizwa **kuthibitisha** udahili wao katika chuo kimojawapo **kuanzia leo tarehe 09 hadi 17 Oktoba, 2020** kwa kutumia ujumbe mfupi wenye namba maalum ya siri uliotumwa kupitia namba zao za simu au barua pepe walizotumia wakati wa kuomba udahili. Wale ambao hawatapata kwa wakati ujumbe huo, wanashauriwa kuingia kwenye mifumo ya udahili ya vyuo walivyodahiliwa na kuomba kutumiwa ujumbe mfupi wenye namba maalum ya siri ili kuweza kujithibitisha katika chuo husika.

Uthibitisho wa udahili ufanyike kupitia akaunti ambayo muombaji alitumia wakati wa kuomba udahili. Orodha ya majina ya waombaji waliodahiliwa katika chuo zaidi ya kimoja imewekwa kwenye tovuti ya TCU (www.tcu.go.tz).

3.0 KUFUNGULIWA KWA AWAMU YA PILI YA UDAHILI 2020/2021


Tume inatangaza kuwa **Awamu ya Pili ya udahili wa Shahada ya Kwanza kwa mwaka wa masomo 2020/2021 itanza rasmi Jumatatu tarehe 12 hadi 18 Oktoba, 2020**. Tume inasisitiza kuwa waombaji ambao hawakuweza kutuma maombi ya udahili au hawakudahiliwa katika awamu ya kwanza kutokana na sababu mbalimbali watumie fursa hii vizuri kwa kutuma maombi yao ya udahili kwenye vyuo wanavyovipenda. Tume inaelekeza Taasisi za Elimu ya Juu kutangaza programu ambazo bado zina nafasi. Aidha, waombaji na vyuo wanahimizwa kuzingatia utaratibu wa udahili kwa Awamu ya Pili kama

ilivyooneshwa kwenye kalenda ya udahili iliyotolewa na TCU kama inavyoonekana kwenye tovuti ya TCU (www.tcu.go.tz).

4.0 WITO KWA WAOMBAJI UDAHILI

Waombaji udahili wa Shahada ya Kwanza wanakumbushwa kuwa masuala yote yanayohusu udahili au kujithibitisha katika chuo kimoja yawasilishwe moja kwa moja kwenye vyuo husika. Kwa wale ambao watapata changamoto katika kujithibitisha, vyuo vyote vimeelekezwa kupokea taarifa zao na kutafuta ufumbuzi wa haraka kwa kuzingatia miongozo na taratibu zilizowekwa.

Imetolewa na:



Prof. Charles D. Kihampa
KATIBU MTENDAJI
TUME YA VYUO VIKUU TANZANIA